**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**GISAMBALANG SHULE YA SEKONDARI**.

SHULE YA SEKONDARI GISAMBALANG,

S.L.P 251,

BARUA PEPE:gisambalang@gmail.com

CELL PHONE: 0787 145 039/0689 708 323

TAREHE: ***24 November 2021***

Kumb Na…….

Jina la Mwanafunzi…….....

S.L.P 251.

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GISAMBALANG, WILAYA YA HANANG, MKOA WA MANYARA KWA MWAKA WA MASOMO 20…...**

*1.0* ***Utangulizi***

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza (I)** katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2022.Shule ya sekondari Gisambalang ipo umbali wa **km 48** kusini mwa halmashauri ya wilaya Hanang au mji wa katesh.

Usafiri wa mabasi ya uma kutoka mji wa katesh unapatikana katika kituo cha mabasi cha katesh.Nauli ni ***Tsh. 3,000/=***

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe…….Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe……na mwisho wa kuripoti ni Tarehe……Ndani ya siku saba.

***2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia***

***2.1 Sare za shule***

- Wavulana: Suruali mbili (2) nyeusi na shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mifupi.
- Wasichana: Sketi nyeusi mbili (2) ziwe ndefu kupita magoti na iwe na mistari 16 tu, shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya Kamba (pair mbili) kwa wavulana na wasichana.
- Soksi nyeupe mbili kwa wasichana na soksi za kaki mbili kwa wavulana.

***NB: Maelezo ya mshono (Suruali na sketi ziwe na malinda.)***

- Sweta mbili (2) kwa mwanafunzi zenye rangi ya damu ya mzee.
- Rangi ya hijab ifanane na sare za shule(ambatanisha mshono)
- **2.2 sare za michezo**

- Wavulana:bukta 2 na T-shirt nyekundu 2
- Wasichana:bukta 2 na T-shirt nyekundu 2 / Track suit kwa waislam au wanaopenda (Rangi nyekundu)

2.3 Daftari kubwa kumi(10) (counter books) na daftari ndogo kumi (10) ,kalamu na mkebe wa hesabu.

2.4 chakula cha wanafunzi wa kutwa,nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.5 mzazi/mlezi zingatia mahitaji mengine kwa mwanao.

**3.0 sheria na kanuni muhimu za shule ya sekondari Gisambalang**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu . Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili/ mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
i) Kutunza mali za umma.
j) Mwanafunzi haruhusiwi kufika nyumba za walimu bila idhini/ruhusa.

## 3.2 Makosa yafuatayo yanaweza yakakusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

(a) wizi

(b) uasherati na ushoga

(c)ubakaji

(d)ulevi na matumizi ya dawa za kulevya Kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.

(e) kupigana au kupiga.

(f)kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) kudharau Bendera ya Taifa.

(h)Kuwa mjamzito/kupata mimba.

(I) kuoa au kuolewa.

(j)kutoa mimba.

(k)kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.

(l)kukataa adhabu kwa makusudi.

(m) kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:-

(a) Medical Examination form ambayo itajazwa no Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule Mara utakaporipoti shuleni.

(b)Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na Makosa ya jinai.

(c)Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo Mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA  SHULE HII**

**----------**

**MKUU WA SHULE**

SHULE YA SEKONDARI GISAMBALANG

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE:**

Mkuu wa shule,

Shule ya sekondari Gisambalang,

S.L.P 251,

Katesh,Hanang.

Manyara.

## A.MWANAFUNZI:

Mimi.....nimesoma kwa umakini barua ya maagizo ya kujiunga na shule yako.

Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaikubali/ninaikataa nafasi hiyo kwa sababu.....

Pia nayakubali/nayakataa ***MASHARTI*** na sheria za shule yako.Ninaahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na Makosa ya jinai- Makosa Kama hayo yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule, hivyo nikishiriki Makosa hayo nifukuzwe shule.

Tarehe……  Sahihi……

## B: MZAZI/MLEZI:

Mimi.....mzazi/Mlezi wa.....ambaye amechaguliwa kujiunga na shule yako,nimesoma maagizo ya kujiunga na shule yako, ninaikubali/ninakataa nafasi hiyo.Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule yako katika muda uliopangwa,pia nitashirikiana daima na shule yako katika kumkuza mtoto na kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake, wazazi na Taifa kwa ujumla.kama unakataa to sababu.....

Ninaahidi mwanangu kutoshiriki katika migomo, fujo na Makosa ya jinai.mwanangu akishiriki Makosa hayo afukuzwe shule.

Saini mzazi/Mlezi..... tarehe.....

N.B.Udanganyifu wowote ambao utasababisha/lenga kumkosesha mwanafunzi masomo/shule hautavumiliwa.

Jina na anwani ya mzazi/mlezi:.....

Namba ya simu.....

*Futalisilohusika.(Tafadhali uje na Fomu hi ikiwa imejazwa vizuri).

**IJAZWE NA MGANGA MKUU/WILAYA/KITUO CHA AFYA.MWANAFUNZI AJE NAYE NA KUMPA MKUU WA SHULE (Usipimweo KWINGINEKO KWINGINE KOKOTE)**

Mimi (jina la Mganga mkuu wa mkoa /wilaya/kituo Cha afya).....

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina mwanafunzi ) .....

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo/ Hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

## A. HALI YA MWILI

1. Mapigo ya moyo.....
2. Kiasi Cha damu.....
3. kundi la damu.....
4. Mkojo.....
5. Kinmoyo.....
6. Masikio.....

ANGALIA Weka maoni yako kuhusu kila kipengele tajwa.

## B. MAGONJWA

Amewahi / Anayo /hana magonjwa yafuatayo;

(a) pumu

(b) kifua kikuu

(C) kifafa

(d) shinikizo la damu chini /juu

(e) vidonda vya tumbo

(f) sickle cell anaemia

(g) ukoma

(h) maradhi ya akili

(I) maradhi Mengineyo makali yasiyotajwa hapo juu.

SAHIHI NA MUHURI WA DAKTARI/ MGANGA

TAREHE.....

***kata lisilotakiwa***

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**

**GISAMBALANG SHULE YA SEKONDARI**.

SHULE YA SEKONDARI GISAMBALANG,

S.L.P 251,

BARUA PEPE:gisambalang@gmail.com

CELL PHONE: 0787 145 039/0689 708 323

TAREHE:…….....

**Kwa Mzazi / Mlezi**

**Wa.....**

**YAH: MAHITAJI MUHIMU YABKUFIKA NAYO SIKU YA KURIPOTI MWANAO SHULENI**

Siku ya kumleta mwanao kujiunga nakidato cha kwanza, Hakikisha unakuja na vitu vifuatavyo bila kukosa haya kimoja ;

**1.mahindi kilo ishirino(20Kg)**

**2. Maharage kilo tank (5kg)**

**3. Fedha Tsh elfu ishirini na mbili (22000 Tsh)**

**4. Sahani moja, bakuli moja, na kijiko kimoja**

Atakapofika mwezi Wa saba (July), 2022 utaleta vitu vifuatavyo:

**1 .Mahindi kilo sitini namoja(61kg)**

**2. Maharage kilo ishirini na tano (25kg)**

**3. Fedha za kitanzania elfu ishirini na mbili (22000/=)**

**Wako katika ujenzi**

**Sahihi.....**

HASAN MOHAMME( KATIBU)